# MAONI & U

## Nukuu



Iwapo maisha yangekuwa yanatab

Eleanor Roosevelt, mwanasiasa na mw

## Madai ya madereva malori yatafutiwe suluhu mapema

Jana, gazeti hili liliandika habari kuhusu vuguvugu la mgomo wa madereva wa malori linaloripotiwa kuandaliwa kichinichini, ikiwa ni kengele ya tahadhari kwa Serikali na mamlaka husika, waajiri na wadau wote wa sekta ya usafirishaji.

Badala ya kusubiri mgomo huo utokee na kusababisha madhara kwa uchumi na huduma mbalimbali, ni wakati mwafaka kwa Serikali kukutana na vyama vya madereva, wamiliki wa malori na wadau wengine ili kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili.

Sekta ya usafirishaji wa mizigo ni mhimili muhimu wa uchumi wa Tanzania. Malori husafirisha bidhaa kutoka bandarini kwenda mikoa mbalimbali na nchi jirani na kinyume chake; huku yakibeba mazao, vifaa vya viwandani, pembejeo za kilimo na bidhaa muhimu zinazotegemewa na wananchi kila siku.

Tanzania pia ni lango muhimu la biashara kwa nchi kadhaa zisizo na bandari kama Zambia, Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Hivyo, usumbufu wowote katika sekta ya malori unaweza kuathiri si Tanzania pekee, bali pia biashara na uchumi wa nchi jirani zinazotegemea huduma za usafirishaji kupitia nchi yetu.

Ndiyo maana taarifa za kuwapo kwa vuguvugu la mgomo zinapaswa kushughulikiwa kwa umuhimu. Serikali inapaswa kuona dalili hizi kama fursa ya kuzuia mgogoro kabla haujakua, badala ya kusubiri hali ifikie hatua ya kusimama kwa shughuli za usafirishaji. Mara nyingi migogoro ya kikazi huanza kwa malalamiko yanayopuuzwa au kucheleweshwa kufanyiwa kazi. Kadiri muda unavyopita bila majibu ya kuridhisha, ndivyo hali ya kutoridhika inavyoongezeka na hatimaye kusababisha hatua kali zaidi.

Madereva wa malori wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali kwa muda mrefu. Zipo zinazohusu mazingira ya kazi, muda mrefu wa safari, uchovu unaotokana na kuendesha kwa saa nyingi, masuala ya usalama barabarani, huduma katika maeneo ya mapumziko na masilahi yao kwa ujumla.

Hata kama si madai yote yanaweza kutekelezwa kwa wakati mmoja, ni muhimu wahusika wakasikilizwa na kupewa nafasi ya kueleza changamoto zao kupitia majukwaa rasmi.

Kinachoongeza umuhimu wa hatua za haraka ni kuwa hali kama hiyo inaweza kusababisha upotoshaji wa taarifa, kuzua taharuki na kufanya iwe vigumu kwa mamlaka kujua kwa usahihi madai yanayowasilishwa.

Pale ambapo hakuna njia rasmi za mawasiliano kati ya wadau na mamlaka, nafasi ya uvumi na taarifa zisizo sahihi huongezeka. Serikali inaweza kuondoa hali hiyo kwa kuanzisha mazungumzo ya wazi yatakayowakutanisha wadau wote muhimu.

Tunaona ni vyema Serikali kupitia wizara, taasisi za usafirishaji na mamlaka za kazi kuitisha kikao cha pamoja na vyama vya madereva, wamiliki wa malori, waajiri na wadau wengine wa sekta hiyo. Kikao hicho kisiwe cha kusikiliza malalamiko pekee, bali kiwe mwanzo wa mchakato wa kutafuta suluhisho la kudumu.

Tunashauri haya kwa kuwa mazungumzo ndiyo msingi wa maendeleo ya uchumi. Nchi nyingi zimefanikiwa kudhibiti migogoro ya wafanyakazi kwa kuweka mifumo madhubuti ya majadiliano kabla hali haijawa mbaya.

Tunafahamu kuwa malalamiko mengi hayatekelezwi moja kwa moja na Serikali, lakini yenyewe kama mratibu iyachukue, isisubiri mgomo wa malori utokee ndipo ichukue hatua. Wakati wa kuwakutanisha wadau na kutafuta mwafaka ni sasa, kabla athari zake hazijagusa uchumi na maisha ya wananchi.

Jumatano Juni 03, 2026 Pg6



# Ajali yaua watu saba, kujeruhi 17 Singida

**Na MWANDISHI WETU**

WATU saba wamefariki dunia na wengine 17 kujeruhiwa, baada ya lori kuligonga basi dogo aina ya Toyota Coaster, Mlima Sekenke, wilayani Iramba mkoani Singida.

Ajali hiyo ilitokea jana, saa nne asubuhi, wakati lori hilo lililokuwa likishuka mlimani kupata hitilafu ya mfumo wa breki na kuligonga kwa nyuma basi hilo ambalo lilikuwa likitoka Singida kwenda Igunga, mkoani Tabora.

Magari yote mawili yalitumbukia katika korongo lililopo kando mwa barabara kuu ya Dar es Salaam-Mwanza na kusababisha vifo hivyo na majeruhi.

Naye, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Peter Janga, alisema majeruhi 17 walipokewa katika Hospitali ya Wilaya ya Iramba kwa matibabu zaidi.

Alisema mmoja alipoteza maisha akiwa hospitali, huku jitihada za kutambua miili ya marehemu zikiendelea kufanywa na vyombo vya usalama na wananchi.

"Tumepokea miili ya watu sita ambao walifariki katika eneo la ajali, wanaume wanne na wawili wakiwa watoto wakike na majeruhi 17 ambao mmoja wao alifariki hospitalini,"alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alifika eneo la ajali hiyo na baadaye hospitalini ambapo alitoa pole kwa familia zilizopoteza wapendwa wao na kuwatakia nafuu majeruhi wanaoendelea kupewa matibabu.

Alisema serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya majeruhi na kuchunguza chanzo halisi cha ajali hiyo, kubaini mazingira yote yaliyosababisha kutokea kwake.

Halima aliwataka madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani na kuhakikisha magari yao yanakuwa katika hali nzuri ya kiufundi kabla ya kuanza safari, hususan katika maeneo yenye miteremko mikali kama mlima wa Sekenke.